



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA**



Desemba 06, 2022

Tovuti : www.ludewadc.go.tz

TANGAZO

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ludewa inapenda kuwatangazia wananchi wote wa Wilaya ya Ludewa kuwa, kuanzia tarehe 01 mwezi Desemba hadi tarehe 09 Disemba 2022 ni wiki ya maadhimisho ya sherehe za uhuru ambayo kilele chake ni tarehe 09 Desemba, 2022.

Shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufanyaji usafi wa mazingira kwenye maeneo yote ya Wilaya ya Ludewa, upandaji miti ya maji, matunda na miti ya kivuli pamoja, mashindano ya michezo yote, utoaji wa msaada wa kisheria na elimu ya mapambano ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia yatatolewa katika uwanja wa mpira wa Halmashauri.

Kesho tarehe 07 na tarehe 08 Desemba ni siku za michezo mbalimbali ikihusisha michezo ya kukimbia, michezo ya mpira wa miguu, mashindano ya ngoma za asili na mazoezi ya viungo vya mwili ikiongozwa na **LUDEWA FITNESS CLUB**.

Sambamba na hayo kwa siku mbili hizo kutakuwa na zoezi la upimaji magonjwa yote bure, utoaji wa msaada wa kisheria na Dawati la Jinsia watahiriki kutoa elimu juu ya mapambano ya ukatili na unyanyasaji.

Na tarehe 09 Desemba 2022 ndio siku ya kilele cha maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru, siku hiyo kuanzia saa mbili kamili asubuhi kutakuwa na matukio mbalimbali ikiwa ni pamoja na Maandamano, Midahalo, uwasilishaji wa taarifa ya mafanikio ya miaka 61 ya Uhuru ndani ya Wilaya ya Ludewa na Uzinduzi wa Kauli mbiu ya Wilaya ya Ludewa.

Viongozi wa Serikali za Vijiji, Kata na Wananchi wote wa Wilaya ya Ludewa kwa ujmla wake mnakaribishwa kushiriki siku hii muhimu ili kuona mafanikio ya Wilaya ya Ludewa kwa miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika (Tanzania Bara).

Wote Mnakaribishwa.

Chrispin B. Kalinga
Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.